

SEKTA YA MALIASILI:

1.1: UTANGULIZI:

Kwa mfumo wa Serikali za Mitaa, Idara ya Maliasili inajumuisha; Mimitu, Nyuki, Wanyamapori, Uvuvi, Utalii mambo ya kale na Mazingira.

Lakini katika utendaji kazi, kila sekta ina sera inayoongeza kufanya kazi zake K.m. Sekta ya Wanyamapori – ina sera ya wanyamapori ya 1997, Uvuvi 1997, Mimitu 1998, Nyuki 1998 n.k ambazo huko nyuma hazikuwepo, na kama zilikuwepo, zilikuwepo hazikuwa SHIRIKISHI. Vilevile kila sekta inasheria zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yake.

2.0: MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU

Siasa, ulinzi, Utawala na kiuchumi, Idara hii imepitia mabadiliko mengi kimuundo ambapo imesababisha kupatikana kwa sera mpya, sheria mpya na program za utekelezaji wake. Kwa mfano;

- Wanyamapori – kuna ushirikishwaji wa jamii katika Uhifadhi wa Wanyamapori kwa mfano wa Wildlife Menagement Areas – katika mapori ingefaa.
- Kuna ulinzi Shirikishi wa Wanyamapori na Rasilimali za Uvuvi (Bead Manegement Units).

- Misitū, kuna Usimamizi Shirikishi wa Misitū (PFM)

3. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA NA SEKTA ZILIZOPO

3.1 MAFANIKIO:

- Kila sekta ina sera, Sheria mpya na Mipango ya utekelezaji Shirikishi.
- Mbinga – Pori la Hifadhi la wanyamapori la Akiba la Liparamba.
- Misitū; tuna misitū ya Hifadhi ya jamii 17 yenye ukubwa wa Hekta 33,000.
- Wananchi wanaelimu na na ufahamu wa kutosha kuhusu ulinzi, usimamizi na uendelezaji Maliasili zetu.
- Upandaji miti – Idadi ya ukuzaji miti imeongezeka toka lengo la 250,000 mpaka 6,000,000 miche kwa mwaka.
- Ufugaji wa samaki – umeanza na kuendelezwa na wananchi wenyewe. Kuna wastani wa mabwawa ya kufugia samaki yapatayo 500.
- Matukio ya wanyama kudhuru binadamu/mifugo yamepungua sana kutokana na ulinzi Shirikishi na elimu kwa umma.
- Matumizi ya Mitumbwi ya kisasa imeongezeka sana na kupungua sana kwa mitumbwi ya magome na ajali za majini.
- Maeneo mengi ya vivutio vya Utalii na Utalii wa Utamaduni yametambuliwa. Katika kulinda Mazingira, vyanzo vikuu vya maji vimetambuliwa na usimamiwa

kisheria. k.m. vyanzo 60 vimepimwa, kuwekewa mipaka na kutungiwa sheria ndogo.

3.2. FURSA ZILIZOPO:

- Watu wenye uwezo wa kufanya kazi wapo.
- Tuna maeneo yenye maji, Ziwa Nyasa, mito Mikuu, Lumeme, Ruhuhu, Ruhekei, Lunyele, Mungaka, Ruvuma n.k. ambayo inaweza kutumika kwa shughuli za Uvuvi, Ufugaji wa samaki pamoja na maendeleo ya wanyama na upandaji miti.
- Mapori yanayoweza kutumika kwa ufugaji wa nyuki, kulinda wanyamapori.
- Kuna vivutio vya Utalii, Jiwe la Mbuji, Mialo ya Kwambe, Kilosa n.k. kuna Hifadhi ya Wanyamapori, Mapango ya kale ya makoro, Matiri, Lilangangondo huko Namswea.
- Maeneo ya kufanya”Camping” kwa watalii watembeo kwa miguu (Walking safaris).
- Tuna madini mengi kama makaa ya mawe, vito na dhahabu.

4.0: CHANGAMOTO ZA IDARA:

- ✓ Uhaba wa watumishi wenye ujuzi wa kutosha kufanya kazi.
- ✓ Uhaba wa vitendea kazi, wakati mwingine hakuna.

- ✓ Ufinyu wa bajeti ya kuwezesha Idara kufanya kazi zake.

5.0: MATARAJIO:

Mabadiliko makubwa baada ya uzalishaji wa watumishi, vitendea kazi na kuongezeka kwa bajeti ambavyo vitapelekea kukuza na kuboresha shughuli za Idara kwa ujumla.